**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**4 Oktoba 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe
Aseli Wilison
Bashiri Rashidi
Beda John Mkusu
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rwechungura
George Kabogo
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Mejah Mbuya
Paulo Atibu Hatibu
Ramadhani Rajabu Nyengo
Shamte J Kigoma

**Msafara wa Baiskeli**

Ubalozi wa Ireland wamekubali kudhamini msafara. Wakalishi wao anayeitwa Nigel alimpigia simu Elaine na alisema amtumie badjeti wiki ijayo. Tuliandika badjeti pamoja kwenye mkutano.

Mwanake mwenye kampuni ya Guta alisema watachangia guta lakini bora tupate taarifa kutoka mwenye kampuni mwenyewe pia.

Juma alitoa repoti kwamba Bwana Abdul wa Bakhresa alisema kwamba maombi yetu yalienda kwa Bwana Lawrence wa Bakhresa. Elaine alimpigia simu Bwana Lawrence na yeye alisema bado hajawasiliana na Bwana Bakhresa kuhusu hiyo na labda tutapata jibu wiki ijayo.

Bado hatuna hakika kuhusu mchango wa ubalozi wa China. Mejah atafuatalia wiki hii.

Mejah pia atafuatalia na Ultimate Security kuhusu ambulance.

Manispaa ya Ilala walimpigia simu Mejah na walisema tulipe ada ya kutumia Mnazi Mmoja. Mejah atakutana naye Jumatatu kueleza kwamba tunaomba kupata bure kama mwaka jana, na mgeni rasmi yetu ni Azzan Zungu Mbunge. Juma aliomba Councillor Lupilya kutusaidia kupata sehemu bure na alisema tuandike barua kualika mkurugenzi wa manispaa ya Ilala na atatusaidia.

Elaine atachapa barua za mwaliko kwa ajili ya mashirika tunashirikiana nao kuwaalika kwenye msafara. Tualike JEMA, shirika la mazingira chuo kikuu, Kali Mata na Mama Wamba.

Mejah atafuatalia kupata matangazo kwenye magazeti na redio kabla ya msafara.

Elaine atachapa bango na vipeperushi.

**Watafiti**
Filbert, Juma, Aseli na Paulo walisaidia watafiti – walitembea nao na baiskeli, waliwasaidia kusanya savei na walipata watu kujaza savei. Filbert alisanya savei na atawapa watafiti. Elaine ataweka habari kwenye website.

**gTKP Mkutano Cameroon**
Mejah alitoa repoti kuhusu kutembelea Cameroon kushiriki kwenye warsha ya utawala wa sekta ya usafiri. Watanzania wawili wengine walikuwepo – Ronald Lwakatawe kutoka Road Fund (aliyemwakilishi Joseph Haule) na Mr Awal wa TARA.

Mejah alitoa maada siku ya pili na watu waliipenda.

Masuala kwenye warsha yalikuwa mpango kuandika kitabu kusaidia watu non-technical kwenye NGOs kuchangia mawazo katika sekta ya usafiri, mabadaliko ya majira, ushirikiano na vyombo vya habari, vipi kuhakikisha hela za barabara zinatumikwa vizuri na mambo ya kusanya takwimu. Tuliongea kwamba tupate wanafunzi wa chuo kikuu kama wanachama ili watusaidie kusanya takwimu.

Mejah ataandika repoti kuhusu warsha wiki hii. Elaine atascan photos zilizopigwa kwenye warsha na ataweka habari kwenye website.

**Mkutano wa UNEP, Kenya**
Kwenye mkutano wa Cameroon Mejah alialikwa kwenda mkutano Nairobi, Kenya tarehe 21-23 Oktober kuhusu ubora wa hewa kwenye maeneo ya jiji. Mejah alisema atapenda mwanachama mwingine apate nafasi kwenda lakini Elaine na wanachama wengine walipendekeza bora Mejah aende kwa sababu alituwakilishi vizuri Cameroon, na mkutano wa Nairobi itakuwa technical na wa kisayanzi kuhusu ubora wa hewa. Mejah atajaza fomu ya kuhudhuria wiki hii.

**Siku la usalama barabarani Morogoro**
Elaine alipigiwa simu na mtu anayeitwa Allan Jones ambaye ni consultant anafanya kazi na wizara ya miundombinu. Alisema kwamba kuna tukio la usalama barabarani Morogoro na amesikia kwamba tuna mradi wa kufundisha usalama barabarani kwa wapanda baiskeli. Elaine alisema kwamba wanachama wetu wameshapata mafunzo na wanaweza kufundisha. Alimwalika kwenye mkutano wa leo lakini hakuweza kuhudhuria. Alisema atapenda kutana nasi wakati wa wiki na alipendekeza chuo kikuu jumatatu saa saba. Filbert, Paulo, Hussein Hamza, Bashiri na Shamte walisema watakuja chuo saa sita na nusu mchana kutana naye pamoja na Elaine.

**Mambo ya hela**
Matumizi na mapato tangu 13 Septemba:
Juma alikuwa na Tsh 41,900 ya hela ya UWABA tarehe 13 Septemba

Mejah na Juma walichukua Tsh 70,000 kutoka benki na Juma alichukua Tsh 60,000 kama advance ya posho ya miezi mitatu na Mejah alichukua Tsh 10,000 tena ya hela ya simu, ambayo bado hajatumia lakini atatumia wiki hii.
Tulipata Tsh 7,000 ya hela ya guta wiki mbili iliyopita
Tulipata mchango wa Tsh 20,000 kutoka kwa Sarah anayefanyakazi Femina.
Tsh 12,000 ilitumikwa na Juma kwa hela ya simu
Tsh 2,000 ilipewa na Juma kwa Juma Chibaya, mwenye nyumba wa ofisi, kama advance
Tsh 2,700 ilitumikwa kwa ajili ya chakula kwa Juma na Filbert siku walifanya savei
Tulipata Tsh 7,000 ya hela ya guta leo.

Juma sasa ana Tsh 59,200 ya hela ya UWABA.

**Mambo mengine**

Elaine alileta makala kuhusu mradi wa "Pedalling for Life" unaoendeshwa na padre Phillipines – wadereva wa baisikeli za teksi za gurudumu tatu (pedicab) wanawezeshwa kununua pedicab yao kwa kulipa kidogo kidogo. Tuliongea kuhusu kuanzisha mradi kama huu kwa wadereva wa guta kununua guta lao.

**Masuala kufuatalia baada ya msafara:**

- Kumwalika Mama Wamba kwenye mkutano
- Kuanza kufundisha wanafunzi wa shule kwenye mradi wa Wamba
- Kufuatalia kuhusu kongamano na diwani Lupilya, pia kuangalia kama benki ya dunia wanaweza kulipa
- Kutana na TARA
- Kuomba wizara ya miundombinu tuwe kwenye orodha ya washika dau
- Kuomba EU kutengeneza sera kuhusu usafiri wa siyo wa moto
- Kukagua barabara mpya tatu
- Kufuatalia kuhusu daraja la Kigamboni
- Kutana na Foundation for Civil Society
- Kutumia barua kwa TANROADS kushukuru kwa marekebisho ya njia za baiskeli Nyerere Road
- Kutana na road fund